

- Kufuta utaratibu wa kuwatoza wananchi fedha wanapotaka barua za Utambulisho kwenda katika vyombo vya dola (Polisi, mahakamani, n.k.).

Chama Cha Wananchi – CUF kinapenda kila mwananchi afahamu:


Kwamba ili haya yaweze kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kujenga misingi mipya ya maendeleo itakayomuwezesha kila Mtanzania kuishi kwa furaha na amani ni lazima wananchi wenyewe watoe ridhaa hiyo kupitia kura zao kwenye chaguzi zijazo.

Chama Cha Wananchi – CUF kinaamini ushirikiano wake na Umma wa Tanzania ambao umejengeka na kuwa imara zaidi katika kipindi cha miaka mitano hii kitaendelezwa na kila anayeitakia mema nchi hii katika Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2020 baada ya wananchi kuona matunda ya kazi za serikali mpya za mitaa za CUF- Chama Cha Wananchi.

Chama Cha Wananchi – CUF, Chama imara na makini ambacho siku zote kimekuwa msitari wa mbele kupigania haki za wananchi za kuondokana na maisha ya hofu ambayo yamejengwa na utawala uliopo kwa muda mrefu sasa. Kazi hii ili iweze kutekelezwa ni lazima tupige kura zetu na kuhakikisha tunazilinda na mwisho kuhakikisha wale tuliowachagua kwa ridhaa zetu wanatangazwa kushika madaraka, Chama kitakuwa pamoja na wananchi.

Wakati umefika TUENDELEZENI USHIRIKIANO WETU ili tupate matunda ya mageuzi na mabadiliko na DAIMA TUSIKUBALI KUGAWANYWA.

**HAKI SAWA NA FURAHA KWA WOTE**



**THE CIVIC UNITED FRONT**  
(CUF - CHAMA CHA WANANCHI)

**ILANI YA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA 2019**



**HAKI SAWA NA FURAHA KWA WOTE**

## **TUENDELEZE USHIRIKIANO WETU:**

Chama Cha Wananchi- CUF siku zote kimekuwa msitari wa mbele kushirikiana na Wananchi katika kuleta Mabadiliko ya Msingi katika nchi yetu, mabadiliko ambayo yatawezesha wananchi kujikomboa kutoka katika matatizo yao ya msingi na kuwa na maendeleo ya Kiuchumi yatakayowezesha kukidhi mahitaji muhimu katika maisha yao ya kila siku.

Katika dunia ya sasa Mataifa mengi ikiwa ni pamoja na yale makubwa yamekuwa yakizitumia serikali za mitaa kushughulikia matatizo ya msingi katika maeneo yanayozizunguka jamii zenyewe na kuyaacha yale mambo makubwa yashughulikiwe na serikali kuu ambayo ndiyo yenye uwezo mkubwa zaidi.

Jambo la kusikitisha tangu mfumo wa Vyama Vingi uanzishwe hapa nchini takriban miaka 27 iliyopita serikali za mitaa ambazo nyingi zinaongozwa na chama tawala zimeshindwa kabisa kutumika kuwa nyenzo za maendeleo ya wananchi na badala yake zimekuwa zikitumika kama nyenzo za kuwatisha wananchi, na kuwachangisha michango mbalimbali isiyokuwa na maana, kujifanya mahakama zisizo rasmi, kuwajengea wananchi hofu kwa vitisho vya mara kwa mara, wakati mwingine kupora viwanja, majumba, mashamba na mali za wananchi wanyonge. Chama Cha Wananchi – CUF kinawaomba wananchi kuendeleza na kuimarisha ushirikiano mzuri uliojengeka baina yetu na kukiwezesha Chama kushinda uchaguzi wa mwaka huu wa Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji ili tuweze kufanya mambo ya msingi wakati tukisubiri kuendeleza ushirikiano wetu katika Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Chama Cha Wananchi – CUF kikishinda Uchaguzi huu, kitaanzisha utaratibu mpya utakaowezesha serikali zetu za mitaa kufanya yafuatayo:-

- Kuondoa hofu na vitisho vinavyoelekezwa kwa Wananchi;

- Kuanzisha utaratibu mzuri wa kusuluhisha migogoro ya wananchi badala ya kuwatisha, kuwajengea hofu na hatimae kujifanya Mahakama zinazoishia kuwadhulumu mali zao;
- Kujenga shule za awali, vituo vya kulelea watoto wadogo na yatima;
- Kujenga Zahanati , vituo maalum vya uzazi na kliniki za watoto;
- Kujenga madarasa; mengi yenye ubora.
- Kusimamia kwa kuanzisha utaratibu wa kuwapa chakula wanafunzi wote wakiwa shuleni ili waweze kufuatilia masomo vizuri;
- Kusimamia usambazaji mzuri wa chakula cha msaada kwa walengwa wakati wa maafa;
- Kuweka utaratibu wa kuwapatia wanafunzi wote virutubisho muhimu kama vile Vitamin A (inayoongeza kinga ya mwili na kuzuia uharibifu wa macho) na dawa za kuzuia minyoo;
- Kuwasaidia wakulima kupata pembejeo kwa bei nafuu;
- Kusimamia wakulima kupata masoko bora ya mazao yao na kuondoa makato yasiyo na msingi;
- Kulipia ada za wanafunzi wasiojiweza waliopata nafasi za kuendelea na masomo ya juu;
- Kusimamia utaratibu wa kugawa vyandarua vilivyowekwa dawa kwa kina mama wajawazito na watoto wadogo;
- Kusimamia na kufuatilia upimaji wa mashamba na viwanja vya wananchi ili waweze kupata hati za kumiliki maeneo yao na kuondokana na utaratibu mbovu wa sasa unaowapa wenyeviti wa vijiji na watendaji madaraka ya kupora ardhi zao;
- Kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na haki ya kuabudu dini na madhehebu ayatakayo;
- Kufuta michango ya mwenye;